**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Wilayah Jordan**

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وعد الله الذين آمنوا منكم وعملوا الصالحات ليستخلفنهم في الأرض كما استخلف الذين من قبلهم وليمكنن لهم دينهم الذي ارتضى لهم وليبدلنهم من بعد خوفهم أمنا يعبدونني لا يشركون بي شيئا ومن كفر بعد ذلك فأولئك هم الفاسقون﴾

حزب التحرير

Hizb ut Tahrir

**Jumanne, 22 Dhul-Qa'adah 1443 H** | **21/06/2022 M** | **Na: 1443 / 26**

<u>**Tanzia ya Mbebaji Ulinganizi**</u>

**Mheshimiwa Al-Ustadh Ahmed Muhammad Al-Faqir Al-Ajarmah (Abu Asim)**
**Mmoja wa Mashababu wa Kizazi cha Kwanza cha Hizb ut Tahrir**
**(Imetafsiriwa)**

Kwa nyoyo zenye subira na kuridhia, Hizb ut Tahrir/Wilayah ya Jordan inamuomboleza kwa familia nchini Jordan na Ummah wa Kiislamu, mbebaji da'wah, mmoja wa mashababu wake wema, wasafi na wachamungu, wala hatumtakasi yeyote mbele ya Mwenyezi Mungu, kutoka kizazi cha kwanza cha Hizb ut Tahrir, Ustadh mheshimiwa:

**Ahmed Muhammad Al-Faqir Al-Ajarmah**

Aliyefariki kwenda kwenye rehma za Mwenyezi Mungu Mtukufu mnamo siku ya Jumatatu, tarehe 21 Dhul Qa'adah 1443 H sawia na 20/6/2022, akiwa na umri wa miaka tisini na tatu, na ambaye alitumia maisha yake yote kufanya kazi kwa ajili ya kusimamisha Khilafah kwa bidii na subira akishikilia ahadi na kubeba da'wah licha ya ukongwe wake, na licha ya madhara na ugumu aliokabiliana nao, baadhi yake ikiwa ni katika magereza ya madhalimu, Mwenyezi Mungu (swt) amrehemu mheshimiwa ndugu Abu Asim. Alikuwa mpole, mwepesi, mwenye kuipenda da'wah na mashababu wake, akifanya kazi kwa bidii, mwenye msimamo katika haki, na akifurahia ahadi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Twamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu amghufirie na amrehemu na amkusanye pamoja na Manabii, wakweli, mashahidi na watu wema katika Pepo za neema, na hao ndio marafiki bora, na twamuomba Mwenyezi Mungu aitulize familia yake kwa subira, afueni na faraja njema.

Ewe Mwenyezi Mungu, mrehemu ndugu yetu Abu Asim, yakirimu makaazi yake, panua mlango wake, na umbadilishie mahali pazuri zaidi pa kuishi kuliko makaazi aliyokuwa nayo, na familia bora zaidi kuliko familia aliyokuwa nayo, na utukusanyie sisi na yeye chini ya bendera ya Mtume wako Siku ya Kiyama.

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir**
**katika Wilayah Jordan**

**Tovuti:** www.hizb-jordan.org

**Pepe:** info@hizb-jordan.org

**Ukurasa wa Facebook:** www.facebook.com/hizb.jordan.org

**Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir:**
www.hizb-ut-tahrir.org
**Tovuti ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir:**
www.hizb-ut-tahrir.info